yanafaa kuuzwa kwa utaratibu unaohifadhiwa na sheria kwa kufuatana na mapendekezo ya Rejinali Kamishina katika Mkoa pamoja na Waziri anayehusika. Halmashauri inamlinda mlaji na kumridhisha mkulima kwa kumpa bei ya haki iliyodhibirika, uhakika wa mauzo ya mazao yake, njia nyepesi ya mauzo na inamlinda asinyonywe na watu wa Kati na kumtia moyo kutoa mazao bora. Na wakati huo huo mlaji huwa na hakika ya kupata mazao mazuri, bei nzuri na kiasi cha kutosha; mazao hutolewa yanayoshughulikiwa na Halmashauri mara kwa mara na kugawanywa kwa mpango wa kuridhisha; na kuzuia unyonyaji wa mtu wa Kati.

Halmashauri si kama inashughulika na mazao ya chakula ya nchi hii, bali inajenga taifa kwa kuleta mpango ulio thabiti na unaoridhisha. Ingelikuwa ni mzigo mkubwa kwa mkulima kushughulika na mauzo ya mazao yeye mwenyewe. Ebu fikiria juu ya shida za kuhifadhi mazao katika ghala, usafirishaji, kufukizia dawa katika mazao ili yasishambuliwe na wadudu, kupanga mazao katika madaraja (gredi) kwa kufuata ubora wake, na uuzaji. Halmashauri imemrahisishia mkulima kazi zote hizi. Hivi sasa Halmashauri inatunza ghala Dar es Salaam, Mtwara, Iringa na Dodoma.

Halmashauri inatumia njia mbali mbali za kuuzia mazao yake.

(a) **BEI KAMILI ZILIZOWEKWA**

k.m. uuzaji wa mahindi na mpunga kwa matumizi ya humu humu nchini huuzwa kwa bei zilizowekwa au kwa bei za mkataba.

(b) **KWA KUWAPA "TENDA"**

Kwa wafanya biashara wanaotazamiwa kununua mazao : k.m. mahindi na mpunga unaouzwa nchi za nje huuzwa kwa kuitisha tenda. Kwa mbegu zote za mafuta, pamoja na korosho, ikiwa ni kwa uuzaji wa humu humu au nje ya nchi, huuzwa kwa kuitisha tenda na hasa zaidi huuzwa kwa mnada.

(c) **UUZAJI WA KUFANYA MIKATABA NA WANUNUZI**

(d) **UUZAJI KATIKA MINADA**

k.m. mbegu za mafuta.

(e) **KUUZIANA SERIKALI KWA SERIKALI**

Kwa fedha taslim au kubadilishana na vifaa vingine.

SWALI LA 4.

JE, HALMASHAURI HUENDESHAJE KAZI ZAKE ?

Ni nia ya Halmashauri kufanya mambo kwa njia za ujamaa katika kazi zake zote. Nia hii inatimizwa kwa kuvitumia vyama vya ushirika na shirika za vyama hivyo kama maajenti wadogo na wakubwa.

Mkulima anapouza mahindi yake katika kituo cha kuuzia, mahindi hayo huchukuliwa moja kwa moja mpaka kwenye chama cha ushirika ambacho ni ajenti mdogo wa Halmashauri.

Chama cha ushirika kinayapeleka mazao hayo kwenye ghala ya ajenti mkubwa. Mara yanapokuwa mikononi mwa ajenti mkubwa wa

Halmashauri mazao hayo huwa ni mali ya Halmashauri. Mazao haya hayawezi kuuzwa bila ruhusa ya Halmashauri. Katika sehemu ambazo Halmashauri inazo ghala kama vile Dar es Salaam, Mtwara, Iringa na Dodoma, chama kidogo cha ushirika (ajenti mdogo) au Shirika la Vyama vya Ushirika (ajenti mkubwa) vinaweza kupeleka mazao moja kwa moja kwenye ghala za Halmashauri. Hivi sasa maajenti wote wakubwa wa Halmashauri ni Vyama vikuu vya Ushirika.

SWALI LA 5.

(a) JE, KAZI ZA HALMASHAURI (KAMA VILE HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO) NA SHIRIKA LA VYAMA VYA USHIRIKA ZINATOFAUTIANA NAMNA GANI?

(b) JE, UPO UHUSIANO WA NAMNA GANI KATI YA HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO NA SHIRIKA LA VYAMA VYA USHIRIKA?

Jambo la maana sana ambalo lazima lieleweke ni tofauti kubwa iliyopo kati ya Shirika za Vyama vya Ushirika na Halmashauri ya Mauzo ya mazao. Vyama vya Ushirika ni vyama vilivyoundwa na wakulima kwa hiari yao wenyewe.

Shirika la Vyama vya Ushirika ni mwungano wa vyama vya ushirika kwa haja ya kurahisisha uendeshaji wa kazi za vyama. Kazi zao ni kuchukua nafasi ambayo hapo mwanzo ilichukuliwa na mfanya biashara mdogo katika msululu wa wauzaji. Zaidi ya hayo, ingawa vyama hivyo hujishughulisha na mazao ya nanna mbali mbali yanayolimwa na wakulima, siyo vitaalam. Kwa mfano, Shirika Kuu la Vyama vya Ushirika nchini Tanganyika (The Co-operative Union of Tanganyika) imevizingatia si vyama vya mazao tu, bali hata vyama vya ufundi, mikopo, na vyama vya walaji vinavyofanya kazi nyingi za namna mbali mbali. Zaidi ya hayo vyama vya ushirika haviwezi kutazamiwa kuendesha kazi za kurekibisha bei. Halmashauri za mazao kama vile Halmashauri ya Taifa ya Mazao kwa upande mwingine, zimeanzishwa na serikali kama mkono wake katika shughuli za mauzo ya mazao. Jambo hili ni muhimu sana siku hizi katika nchi inayoendesha uchumi wake kwa mipango, na wananchi hawawezi kuachwa hivi hivi wakitumainia kudra ya Mungu. Halmashauri za mazao zina madaraka ya kuwalazimisha wote au wenye masoko kufuata sheria zake. Halmashauri zinayo nafasi ya kuwa wataalam katika mauzo yaliyo chini ya madaraka yao, jambo ambalo ni la maana hasa na ni gumu kwa upande wa mazao ya kilimo yanayohusika.

Halmashauri ya Taifa ya Mazao ni Halmashauri ya mauzo. Ilichukua madaraka ya mauzo ya mahindi toka Julai, 1963. Toka hapo imepanua madaraka yake juu ya *Korosho* (Marchi - Septemba, 1964), *Mpunga* (Julai, 1964) na *Mbegu za Mafuta* k.m. *Karanga, Nyonyo, Ufuta*, Marchi, 1965, nchini pote na kusimamia uuzaji wa mbata katika

Mikoa ya Pwani na Tanga na *Mihogo* katika Mkoa wa Kigoma, Ruvuma na Tanga. Mazao mengine yaliyopangwa katika orodha, yaani mazao tunayokusudia kuyachukua siku za mbele kwa kufuatana na mapendekezo ya wakuu wa Mikoa, ni Maharagwe ya kigeni, Maharagwe ya kawaida, Nta, Nazi, Viazi Ulaya, Asali, Mtama, Vitunguu, Njegere, Uwele na Viazi Vitamu. Orodha hizi hutungwa na Bunge ambapo sheria zinazotawala utaratibu wa mauzo hutengenezwa na Waziri wa Biashara na Ushirika.

Tukiangalia upande wa Halmashauri za bidhaa tutaona kwamba Halmashauri hizi kwa kawaida hujishughulisha na bidhaa za aina moja tu; kwa mfano Halmashauri ya Pamba na Mbegu za Pamba inayo madaraka juu ya pamba yenyewe isiyochambuliwa inayouzwa na mkulima, pamba iliyochoambuliwa, na mbegu za pamba. Halmashauri ya Taifa ya Mazao, kwa upande mwingine, hujishughulisha na mazao ya namna mbali mbali. Lakini inaonekana zaidi kwamba mazao haya yakichukuliwa thamani ya zao moja moja huwa thamani yao ni ndogo kuliko ile thamani ya zao moja la bidhaa linalouzwa na Halmashauri za bidhaa.

Karibu Halmashauri nyingi zaidi hujishughulisha na mazao yauzwayo nchi za nje au yanayochambuliwa humu humu nchini ili kuyatayarisha kwa mauzo katika nchi za nje.

Na kwa upande wa uhusiano kati ya Halmashauri ya Mazao na Vyama vya Ushirika nadhani hatuna haja zaidi ya kuzidi kutilia mkazo kama tulivyokwisha sema kwamba kuwepo uhusiano mwema kati ya Halmashauri za mazao na Vyama vya Ushirika ni jambo la lazima kabisa maana vyote ni mali ya wananchi.

Nchini mwetu humu tunajaribu kwa bidii iwezekanavyo kurejesha uhusiano mwema kama huu kwa kuinua sifa za biashara ya vyama vya ushirika mbele ya maajenti wa mauzo au bidhaa katika kila hatua. Uhusiano baina ya Halmashauri za Bidhaa za vyama vya ushirika unakaribiana sana. Sehemu kubwa ya Wajumbe wa Halmashauri huviwakilisha vyama vya ushirika.

Zaidi ya hayo, maajenti wote wakubwa wa Halmashauri ni vyama vya ushirika. Katika kila Mkoa tumevipa Vyama vya Ushirika nafasi ya kwanza ya uajenti wa Halmashauri. Zaidi ya hapo maajenti wetu wote, wakiwa ni shirika za vyama vya ushirika au siyo, huvifikiria kwanza vyama vidogo vya ushirika katika kuchagua maajenti wadogo.

Vyama vya Ushirika vinaisaidia Halmashauri kwa njia nyingi; kwanza hufanya kazi kama kiungo muhimu kati ya Halmashauri na mkulima. Na pia vinaisaidia Halmashauri kuendesha kazi zake kwa ustadi zaidi. Kule kusimamia sheria za kuchagua sifa za mazao mazuri

kwa upande wa Vyama vya Ushirika, kunarahisisha kazi ya mauzo ya mwisho na kuinua bei za mazao. Kazi hiyo inamfaidlia mkulima, chama na Halmashauri na kwa kifupi, husaidia uchumi wote wa kilimo. Kadhalika yale mauzo ya haraka husaidia kuvipatia sifa nzuri Vyama vya Ushirika machoni mwa wakulima — wanachama na hii inamaanisha kwamba mazao hutiwa upesi katika magunia baada ya mavuno. Jambo hili pia humsaidia mkulima kwa vile huongezea sifa nzuri za mazao.

SWALI LA 6.

JE, NI MAMBO GANI YANAYOTAWALA BEI ZA HALMASHAURI?

(Bei zitolewazo kwa wakulima)

Halmashauri huyafikiria mambo mengi inapotoa kisio lake la bei ya zao lo lote lile inaloliangalia. Sababu ya kufanya kisio lililo sawa ni ili kumpa mkulima na mlaji uhakika wa bei zitakavyokuwa ili wakadirie mahitaji yao kwa uthabiti zaidi.

Wakulima na viongozi wa wakulima wanaoelewa nguvu zinazotawala matoleo ya mazao na mahitaji ya walaji, mambo yanayofanya bei zishuke na kupanda bila shaka wataiunga mkono mipango ya serikali inayokusudia kuzirekibisha bei kwa kuitumia Halmashauri ya Taifa ya Mazao. Bila ya kuisumbua akili yako kwa kutumia maneno ya kitaalamu juu ya mambo ya uchumi kama vile mlimbuko wa bei, sheria za mauzo na mahitaji, na kadhalika, tutaeleza kwa kifupi mambo yanayotawala utaratibu wetu wa utoaji wa bei. Kwa kawaida bei hupangwa kwa kufuata kiasi cha mazao yaliyopo na mahitaji yalivyo mahala panapohusika (kwa mfano, ni wanunuzi wangapi wako tayari kununua kiasi kadhaa cha zao fulani kwa bei kadhaa kwa wakati fulani, na ni kiasi gani mkulima yuko tayari kutoa kwa bei kadhaa kwa wakati fulani.)

Zaidi ya hapo, huwa tunafikiria zao fulani katika soko la dunia na kiasi cha zao hilo kinachoweza kupatikana na hivyo bei yake itakuwaje katika soko la dunia.

Pia tunazifikiria gharama zote zinazohusika na uuzaji. Ni mambo haya yanayotusaidia katika kupanga bei ya mazao ya namna mbali mbali. Kazi yote hii inahitaji uchunguzi na mipango ya uangalifu. Si kama kwamba tunabunia tu bei wapewayo wakulima kwa mazao yao au bei inayotolewa kwa walaji kwa mazao wanayonunua. Bei zote zinazotolewa na Halmashauri zina baraka za serikali ya watu iliyochaguliwa kwa njia ya kidemokrasi. Kwa hiyo Halmashauri inakupa bei ya haki inayoweza kupatikana wakati wowote wa mwaka kwa kufuata hali ya mambo yalivyo wakati wa mauzo.

SWALI LA 7.

(a) KWA NINI HALMASHAURI HAIMLIPI MKULIMA ZAIDI YA SHS. 34/20 (KWA MAHINDI YA DARAJA LA I NA LA II) KWA KILO 90 KWENYE KITUO CHA AJENTI MKUU ?

(b) JINSI GANI HALMASHAURI INAELEZA TOFAUTI BAINA YA BEI YA UNUNUZI (WA MAHINDI) NA BEI YA UZAJI ?

Ni kawaida kuwasikia watu kadha wakiuliza kwa nini mkulima anapata kima cha Shs. 26/10 tu kwa kila gunia lake la Mahindi ambapo Halmashauri huuza Mahindi ya daraja la I na II kwa kima cha Shs. 46/80.

Tutajibu maswali haya katika sehemu mbili. Katika sehemu ya kwanza tutaeleza sababu inayolazimu mkulima kupata Shs. 26/10 au Shs. 27/- au Shs. 28/-.

Ni lazima ieleweke tokea mwanzo kwamba Halmashauri haimlipi mkulima mkono kwa mkono. Mpango wa kawaida ni kama ifuatavyo :- Halmashauri huwalipa maajenti wake kiasi cha Shs. 34/20 kwa kila gunia lenye uzito wa ratili 90 kutokana na Mahindi ya daraja la *kwanza* na la *pili*; Shs. 31/50 kwa gunia lenye uzito wa kilo 90 kwa Mahindi ya daraja la *tatu*, na Shs. 26/10 kwa gunia lenye uzito wa kilo 90 kwa Mahindi ya daraja la *nne*.

Maajenti wetu wote ni shirika za Vyama vya Ushirika. Bei anayo-ipata mkulima kwa mazao yake inakadiriwa na Shirika la Vyama vya Ushirika likishauriana na Afisa Mkuu wa Mkoa wa Vyama vya Ushirika (R.C.O.) pamoja na Halmashauri. Sasa tukirudia swali la mwanzo kuhusu sababu inayomfanya mkulima apate chini ya Shs. 34/20, tutaeleza kama ifuatavyo :-

Kama ajenti mkuu (Chama cha Ushirika) anapata Mahindi moja kwa moja kutoka kwa wakulima katika magunia yenye uzito ulio sawa kabisa wa kilo 90 kwa kila gunia jipya, ajenti mkuu atamlipa mkulima bei iliyowekwa na Halmashauri zikipunguzwa senti *tatu* kwa kila ratili, na pia ikipunguzwa kadri yoyote ya ushuru wa mazao, gharama za kazi na usafirishaji kutoka mahali pa soko hadi kunako ghala (ada ya

kwanza ya ajenti); gharama hizo haziwezi kuzidi senti *tatu* kwa kilo moja; gharama ya uchukuzi (au usafirishaji kutoka mahali pa soko mpaka kwenye ghala, ushuru wa soko (ukiwapo) unaolipwa kwa Halmashauri ya (utawala) ya Wilaya.

Gharama hizi zinaonyesha tofauti baina ya bei ilipwayo na Halmashauri kwa ajenti mkuu (ambayo ni Shs. 34/20 kwa daraja la I na la II la Mahindi) na bei ambayo ajenti mkuu anamlipa mkulima.

Twawezejaje kueleza mwongezeko huu wa gharama za ununuzi? Baadhi ya watu hutoa rai ya kwamba gharama hizo ni kielelezo cha hali mojawapo katika uchumi, ambapo shughuli zote za ununuzi wa chakula (au mazao) zinashikwa na mtu mmoja (au Halmashauri moja).

Hesabu na uchunguzi kamili hazipo bado ili kulijibu swali hili kwa ukamilifu. Walakini, sehemu hii ya mwongezeko katika kazi ni mojawapo ya kanuni bora za Uchumi.

Tofauti za bei zaweza kuelezwa mtu akifikiria gharama ndogo ndogo za ununuzi. Wakulima na walaji hawaelewi ni kwa nini Halmashauri hununua kwa bei ndogo na huuza kwa bei za juu zaidi. Wanafikiria kwamba tofauti hii inainufaisha Halmashauri kwa kuiongeza faida. Hii si kweli kwa kuwa gharama zetu za uangalizi (au usimamizi) ni za chini kabisa (kiasi cha $1\frac{1}{2}\%$ tu ya kiwango cha uuzaji). Kiasi kikubwa cha tofauti hiyo huingia katika ushuru na maghala, vyombo, dawa za kufukiza, faida zilipwazo juu ya rasli mali, bima juu ya mazao, vifaa vya kujengea, kupungua (au kunywea) kwa vitu au mazao mbali mbali, ushuru utolewao kwa hazina za tawala za Wilaya, kodi ya maendeleo, gharama za uchukuzi (au usafirishaji) na mizani, na gharama za kuwckea au kulimbikia akiba.

Ni muhimu pia wakulima waelewe kwamba bei tunayowapa ni kubwa zaidi kuliko wangelivyostahili kupata katika bei zinazotolewa na masoko ya dunia. Hii ni kwamba kila tukisafirisha Mahindi nchi za nje, inatubidi kufidia bei zinazotolewa kwa wakulima kwa kuwasaidia, na kwa jinsi hii Halmashauri *hupata* hasara, na nchi pia hupata hasara. Pia ili kuepukana na lazima ya kununua vyakula kwenye ghala za Halmashauri nyakati za shida, ni muhimu wakulima washawishiwe kukadiria ni kiasi gani cha chakula watakihitaji kwa mwaka mzima, na kujiwekea akiba katika ghala zao. Wauze kile tu kinachobakia juu ya mahitaji yao. Kwa kifupi, hizi tofauti zilizopo katika bei za mazao katika masoko ya mumu humu nchini humfanya mkulima awaze kwamba ananyonywa (au kuonelewa). Angalao penginepo wewe na mimi twaweza kuona haki waliyonayo wakulima juu ya mawazo kama hayo, ingawa si katika uhakika halisi — kule kulipa Shs. 46/80 kwa kila gunia la uzito wa kilo 90 (bei ya ghalani), kunahitaji muda mrefu wa maelezo kamili ili kumridhisha mkulima wa kawaida (ingawa kwa kweli si wote) kwamba anapata faida zaidi akilipwa taslim Shs. 34/20 kwa gunia lake lenye uzito wa kilo 90 (daraja la I na II) la Mahindi,

au Shs. 26/10 kwa gunia lenye uzito wa kilo 90 (daraja la IV), kuliko angaliweka Mahindi yake katika ghala, na kufukiza, kununua magunia na kusafirisha hadi kwa mlaji ambaye angekuwa mkazi wa mjini, na kulipwa Shs. 46/80 kwa Mahindi yake yenye daraja la I.

Sasa tutatoa maelezo mafupi kuhusu sababu ziletazo tofauti kati ya bei ambayo Halmashauri hununulia mazao, yaani Shs. 34/20 na bei inayoyauzia, yaani Shs. 46/80.

Halmashauri hugharamia shughuli nyingi kutoka wakati ajenti mkuu anapoyapata Mahindi kwa ajenti mdogo au kutoka moja kwa moja kwa mkulima. Halmashauri humlipa ajenti mkuu kiasi (au kima) cha Shs. 1/30 kwa kila gunia linalonunuliwa. Gharama zingine zinahusu ada za ghala, uwekaji wa rasli mali, gharama au matumizi ya uangalizi (au usimamizi), gharama zaidi za ghala (kiasi cha senti 11 kwa kila gunia liwekwalo kwa wiki moja). Bima, (kutokana na hatari ya moto, mafuriko, na ajali ya Mungu, kutoka wakati mazao yanapopokelewa na kuhifadhiwa ghalani mpaka yatakapotolewa humo, na kadha wa kadha), faida zinazolipwa juu ya fedha za mikopo na rasli mali kupungua au kunywa kwa vitu, akiba itolewayo na Halmashauri kwa kuhifadhiwa akiba, na pia fedha maalum iwekwayo kwa mambo yanayoweza kutokea bila kutazamiwa. Kwa njia hii tunafikia thamani au kiwango chetu cha kuuzia Mahindi ya daraja la I na II kutoka ghalani, baada ya kuongeza gharama zote zilizotajwa hapo juu, (yaani gharama ndogo ndogo za ununuzi au masoko).

Mwishowe utumishi wa mpango au kanuni yoyote ya kukadiria bei ni muhimu ulinganishe kawaida au kipimo cha lengo lililowekwa kufikiwa. Si busara kulifanyia siri jambo hili au utaratibu wowote wa bei. Kipimo chenye maana ni vile tu utaratibu huo unavyoweza kufikia lengo lake, unapotumiwa. Tukiamua kutokana na njia hii, Halmashauri ya Taifa ya Mazao kwa hali zote imefikia lengo lake, yaani katika kurekebisha kanuni ya bei, na ya kwamba kila bei ya masoko ilipotere-mka chini ya bei iliyowekwa, Halmashauri ya Taifa ya Mazao huireki-bisha tofauti hiyo kwa njia ya kuwapa mapato wakulima. Mapato hayo yamenuiwa kuridhisha mambo yafuatayo :-

Kwamba yasibadilike badilike na hali ya uwingi au uchache wa mazao (yaani mapato hayo yarekebisha bei nyakati zote, kukiwa na upungufu au wingi wa mazao), yawazuie wakulima kuweza kujiweka uamuzi usiolingana na hali au matakwa ya muda mrefu, na yasiweze kuzuia kanuni za biashara.

SWALI LA 8.**JE. MAMBO GANI YANAYONUIWA NA HALMASHAURI KATIKA MPANGO WA MAPESA ?**

Ni nia ya Halmashauri kuhifadhi mipango ya fedha za mauzo na ugawanyaji wa fedha zinazosalia baada ya kutoa gharama za matumizi ya mauzo, kati ya wakulima na walaji na mfuko wake wa akiba.

Fedha ya kuendeshea kazi :

Halmashauri inahitaji kiasi fulani cha kuendeshea kazi zake. Fedha zinatakiwa kwa kununulia mazao na vifaa, kusafirishia mazao, na kulipia gharama za mishahara ya wafanya kazi na shughuli za kila siku za kazi zote. Inakisiwa kwamba zitahitajiwa Shs. million 60 wakati wo wote. Fedha zinahitajiwa kulipia thamani ya mazao na vifaa, na utunzaji wa vifaa hivyo na fedha za kujenga ghala. Kiasi cha shilingi milioni 4 kitahitajiwa kwa usafirishaji wa mazao na vifaa, na Shs. laki 3 kwa kutunzia vifaa. Kwa hiyo fedha yote inayohitajiwa si zaidi ya shilingi milioni 20.

Fedha ya Mipango ya Kudumu :

Halmashauri inahitaji kupanua nafasi yake katika mauzo ya mazao, na hasa katika kujenga ghala katika vituo mbali mbali katika nchi nzima. Mnamo miaka mitano ijayo kiasi cha shilingi milioni 16 zitahitajiwa.

Akiba

Halmashauri inahitaji kuwa na fedha ya akiba ya kutumia kwa kufidia hasara zinazoweza kutokea kutokana na shughuli zake za mauzo katika siku za mbele. Fedha yoyote inayosalia kuhifadhiwa kwa njia ya kununua dhamana za serikali.

SWALI LA 9.**JE, MAFANIKIO YA HALMASHAURI NI YAPI ?**

Hapo awali muda si mrefu kabla ya kuanzishwa kwa Halmashauri ya Taifa ya Mazao sehemu nyingi nchini (hasa katika mwaka 1962) zilipatwa na maafa makubwa ya upungufu wa chakula na njaa kutokana na mafuriko ya maji ama ukosefu wa mvua. Msaada wa nafaka hafifu (na maziwa) vilitolewa na Marekani lakini jambo hili halikustahili heshima yetu tukiwa nchi iliyojipatia uhuru wake karibuni; mahala ambapo nafaka ziliweza kupatikana ziliuzwa kwa bei ya juu sana kwa watu waliokabiliwa na maafa ya njaa na mabepari wafanya biashara waliochukua dhiki kama ni bahati waliyopewa na Mungu ya kupandisha bei ili kujipatia utajiri.

Isitoshe, viziwi vyo vyote vilivyokuwepo katika utaratibu wa mauzo vilihusika na mazao yaliyolimwa na W'afrika tu — mataifa mengine yaliachwa huru kujiuzia yatakavyo, na hii ilimaanisha kwamba mpango wowote wa kurekibisha bei ungelipoteza nguvu mara moja. Kuanzishwa kwa Halmashauri kwa kuuza mazao mbali mbali, kushughulika na kuhifadhi na ugawaji wa mazao kungelipunguza matatizo kama hayo. Hivyo Muswada wa Mazao ya Kilimo, (kulinda na kuuza) sheria ya 1962 ilipitishwa na chini ya sheria hiyo Halmashauri ya Taifa ya Mazao (pamoja na Halmashauri nyingine za kuuza mazao) ilianzishwa.

Bila kuwa na kitu chochote cha kuanzia Halmashauri hii imepanuka haraka sana katika muda wa miaka miwili unusu iliyopita. Imeweza kufanikiwa sana katika kulinda na kutimiza utaratibu wa mazao ya chakula nchini na kuondoa tatizo la upungufu wa chakula kwa kuhamisha chakula toka Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine (k.m. Mahindi) au kwa kununua mazao toka nchi za nje (k.m. Mchale). Kwa mazao yanayouzwa nchi za nje kwa sababu ya kusimamiwa kwa uthabiti zaidi na kuhimiza faida ya kuwa na mazao bora, bei nzuri zaidi zimeweza kupatikana kwa Korosho zetu na Mbegu za Mafuta. Mara itakapolazimu kiklogo kidogo tutayatia mazao mengine katika orodha yetu.

Zaidi ya hapo Halmashauri imejenga ghala kubwa mjini Dar es Salaam na Iringa na tunakusudia kupanua nafasi za kuhifadhi mazao katika vituo mbali mbali nchini pote. Inakisiwa kwamba shilingi million 4 zitatumiwa kila mwaka katika muda wa miaka mitatu ijayo, na baada ya hapo shilingi million 2 kila mwaka. Kwa kifupi fedha zozote zilizosalia baada ya kulipia gharama za mauzo zilitumiwa kwa kujengea nafasi nzuri zaidi kwa uhifadhi wa mazao, kuweka akiba katika mfuko wa serikali ili kuiazimisha serikali fedha ya kuendeshea mipango ya maendeleo na kurekibisha bei za mkulima zinapoanguka.

Halmashauri inampatia mlaji (wa humu nchini) mazao bora ya chakula kwa kulisha Taifa. Zaidi ya hayo, kwa sababu ya kuwa na makisio na upeo wa kutabili, akiba ya kutosha ya mazao huhifadhiwa kupambana na shida yoyote isiyotazamiwa siku za mbele. Mwisho Halmashauri inakadiria bei za mazao inayouza kwa kufuatana na mahitaji ya Taifa — siku za nyuma kazi hiyo ilifanywa na bepari mtu wa kati ambaye hakujali matukio mabaya ya bei za juu kwa mlaji mradi alijipatia faida kubwa ajabu. Kwa upande wa vyakula hii ni kazi ya maana sana kwa sababu ikiwa bei za vyakula huwa hazivumiliki kwa jinsi zilivyokuwa na uzito huleta hali ya wasi wasi kwa upande wa siasa.

Kwa mkulima, Halmashauri inamuhakikishia soko. Halmashauri inalazimishwa na sheria za serikali kununua mazao yote yanayoletwa sokoni katika muda uliowekwa, na masharti ya mauzo na bei zilizo-kadiriwa.

Jambo hili ni la maana sana kwa vile hapo siku za nyuma mazao yalikuwa yanasalia hayakununuliwa na mfanya biashara bepari au yalinunuliwa kwa bei ya chini sana. Zaidi ya hayo, kwa kuwa na mfuko wa fedha za akiba za kurekibishia bei, Halmashauri inaweza kununua mazao yote kwa bei za haki na kufanya kipato cha mkulima kiwe sawa. Usafirishaji, uhifadhi na ufukiziaji dawa katika mazao pia ni kazi za Halmashauri. Kwa mulitasari Halmashauri imepata mafanikio mengi katika muda mfupi sana — Halmashauri imewapatia wakulima wa mazao ya chakula — Mahindi, Mpunga — soko thabiti wanapozidisha toleo la mazao zaidi ya mahitaji yao. Tumegawa vyakula kwa njia rahisi inayofaa bila kutetereka na mwisho tumetoa nafasi ya kuhifadhi mazao na tumetoa bei za haki na kuimarisha mapato ya wakulima.

SWALI LA 10.

JE, HALMASHAURI YA MAZAO NI MTU WA KATI?

La hasha, Halmashauri siyo mtu wa kati. Halmashauri hii imeundwa na serikali ili ilifaidie Taifa letu na haifanyi kazi ili kujipatia faida yake yenyewe—ambapo mtu wa kati alikuwa mtu binafsi ambaye alinunua na kuuza mazao ili ajipatie faida kubwa sana. Sasaibu tuzichunguze tofauti zilizopo kati ya Halmashauri ya Taifa ya Mazao na mtu wa kati (Mnyonyaji).

HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO

MTU WA KATI (MNYONYAJI)

- | | |
|---|---|
| 1. Halmashauri imeundwa na serikali na wananchi wenyewe kwa madhumuni ya kuuza mazao. | Mtu wa kati ni mtu au kikundi cha watu binafsi wanaojifanyia biashara yao. |
| 2. Haipati faida. | Mtu wa kati hupata faida. |
| 3. Hufanya kazi bega kwa bega na serikali inapokadiria bei za mazao. | Mtu wa kati hujifanyia bei zake yeye mwenyewe. |
| 4. Hutoa bei zilizo sawa msimu wote. | Mtu wa kati hubadilisha bei kushuka na kupanda mara kwa mara. |
| 5. Huweka akiba ya chakula kati ya msimu wa mwaka hadi msimu wa mwaka mwingine. | Mtu wa kati huficha mazao katika ghala ili kuyauza mazao hayo katika sehemu zilizokabiliwa na maafa ya njaa kwa bei ya unyonyaji wa ajabu na hujipatia faida kubwa. |

- | | |
|--|---|
| 6. Hununua mazao yote yana-
yoletwa sokoni. | Mtu wa kati hununua kiasi cha
mazao anayohitaji. |
| 7. Huitumikia Jamhuri yetu
yote. | Mtu wa kati huwatumikia watu
wachache tu au sehemu moja
maalum. |
| 8. Humwelemisha mkulima. | Hajishughulishi na kumwelemi-
sha mkulima. |
| 9. Huhifadhi kazi za mkulima
na mlaji. | Huwanyonya wote wawili mku-
lima na mlaji. |
| 10. Huwatia moyo wakulima
kutoa mazao mazuri. | Mtu wa kati hajali juu ya uzuri
wa mazao. Mazao yanapokuwa
mabaya yeye ndiyo hufurahi kwa
vile hununua kwa bei ya chini. |
| 11. Ina wajumbe wanaowakili-
sha barabara wakulima na
kila mara husaidia utaratibu
wa Ujamaa. | Hamuwakilishi mtu, ni dalali wa
ubepari. |

SWALI LA 11.

JE, NI MATATIZO GANI YANAYOIKABILI HALMASHAURI HIVI LEO ?

Mbali na mafanikio yaliyokwisha tajwa hapo juu, Halmashauri bado inakabiliwa na shida fulani fulani ambazo kila mara inajitahidi kupambana nazo. Ikiwa peke yake haiwezi kufanikiwa sawa sawa; ni lazima ipate msaada wa ushirikiano kutoka kwa kila sehemu ya watu na hasa wakuu wa Mikoa na Wabunge ambao wakati wote huwa wanakutana na wakulima. Ebu tuyataje baadhi ya matatizo haya :

(a) Upungufu wa ghala za kuhifadhi mazao :

Tatizo hili linaikera Halmashauri na hata Shirika za Vyama vya Ushirika na Halmashauri nyingine. Katika mpango wa Miaka Mitano, tunakusudia kujenga ghala za kutosheleza mahitaji yetu:

(b) Upungufu wa magari na njia za kusafirishia mazao :

Hili ni tatizo la uchumi wetu wote wa Taifa. Kwa zile sehemu zilizokuwa mbali na ghala za maajenti wetu usafirishaji huchukua fedha nyingi zaidi na hivyo hupunguza faida ya mazao kwa wakulima. Tunatumia magari ya Relwe (E.A.R. & H.), Tanga-nyika National Transport Co-operative na magari ya wasafirishaji wengine wa kawaida. Tunajitahidi kwa kadri tuwezavyo kujaribu

kupatana na wasafirishaji ili kupunguza wastani wa gharama za usafirishaji kwa kila gunia. Lakini hata hivyo mpaka sasa ugoi goi katika mauzo ya mazao, kuchelewa na udang'anyifu ni matatizo ambayo ni vigumu kwa Halmashauri kuyamaliza.

(c) Shida za Vyama vya Ushirika :

Halmashauri ni lazima iviimarishe vyama vya ushirika kwa kutoa uajenti kwa vyama vikuu vya ushirika na usabu-ajenti kwa vyama vya ushirika.

(i) Lakini baadhi (au sehemu kubwa) ya idadi ya vyama vya ushirika ni vichanga na kwa kawaida havina ujuzi wa kazi zao, na hivyo tunapovipa vyama uajenti vyama kama hivyo ni uamuzi wa hatari ambao kila mara tunauchukua na wakati mwingine unatutumbukiza katika hasara kubwa. Tunatumaini kwamba kwa kadri vyama vinavyozidi kukua vitahitaji ujuzi zaidi.

(ii) Hata kati ya vyama vya ushirika vilivyokomaa kazi zao za hapo mwanzoni hazikuhusika na uuzaji wa mazao ya chakula kama vile Mpunga na hasa Mahindi, i.e. vilijishughulisha na mazao yasiyo ya chakula tu. Mpaka sasa vyama vingi vya ushirika vinalichukua zao la Mahindi kama zao la pili kwa ubora na hivyo halishughulikiwi kwa uangalifu wa kutosha na kwa makini. Wakuu wa Mikoa na Wabunge wanaweza kusaidia kwa kuvifahamisha vyama vya ushirika na wakulima kwamba mazao ya vyakula ni ya lazima sana kwa maisha bora ya Taifa letu na kwa kweli mazao ya chakula ni ya lazima zaidi kuliko hata mazao tusiyoyatumia kwa chakula bali kwa mauzo ya kujipatia fedha.

(iii) Vyama vya ushirika ni sharti vitambue kwamba ni wajibu wao kushirikiana zaidi bega kwa bega na Halmashauri ya Taifa ya Mazao na kujitahidi kwa kadri viwezavyo kuitangaza na kuwafanya wanachama wao wakulima waipende Halmashauri, kuliko walivyoweza kufanya katika siku za nyuma.

(d) Kupanga na kutoa bei :

Kupanga na kutoa bei hufanywa na Halmashauri na kuthibitishwa na Waziri wa Biashara na Vyama vya Ushirika.

(i) Wakulima na walaji hawaelewi kwa nini Halmashauri inanunua kwa bei ya "chini" (hasa kwa upande wa Mahindi) na inauza kwa bei za juu. Wanafikiria kwamba tofauti iliyopo hutumiwa kwa kutunisha mifuko wa Halmashauri. Hiyo siyo kweli kabisa kwa vile gharama za malipo ya utendaji kazi za Halmashauri ni ndogo sana (ni kama 1½% ya bei ya kuuzia).

Karibu tofauti yote inatumika katika gharama za kukodisha, utiaji wa mazao katika ghala, majengo, vifaa, kufidia hasara zinazotokana na kupungua uzito kwa mazao yanaponyauka na kukauka zaidi, ushuru wa Serikali za Wilaya na Maendeleo, usafirishaji na upimaji na kuweka akiba ya kusaidia kurekibi-sha bei za mazao.

- (ii) Wakulima lazima wafahamishwe zaidi ili waelewe kwamba bei za mahindi tunazowapa ni za juu zaidi kuliko zile wanazoweza kupata katika masoko ya dunia. Hivyo ndiyo kusema kwamba tunapouza Mahindi katika masoko ya dunia huwa ni lazima tuongeze fedha zaidi na hasara hiyo inayotokana na kumfaidia mkulima kwa kufidia upungufu wa bei ya masoko ya dunia ni hasara ya Halmashauri. Na pia kwa kujizuia kununua mazao kutoka kwenye ghala za Halmashauri wakati usiokuwa wa musimu ingelifaa wakulima washauriwe kukisia mahitaji yao ya mazao kwa mwaka mzima na kuhifadhi mazao yao katika ghala zao wenyewe na wauze ile sehemu inayoziditi.

(e) **Kupanga daraja za mazao :**

Wakulima wengi hawaelewi nia, sheria za kupanga daraja za mazao yaani "Grading." Sheria hizi zinasaidia kutuwezesha kupata daraja za mazao na zilizo sawa ili kujipatia bei zilizopo katika masoko ya dunia. Wakulima hufikiri kwamba mpango huu umewekwa kupunguza faida za wakulima (wakati wanapouza mazao ya daraja la chini) ili kuifaidia Halmashauri. Pia siku za nyuma mazao hayakupangwa katika madaraja isipokuwa yale mazao yasiyo ya chakula. Tunajitahidi kwa kadri tuwezavyo kuwaelemisha wakulima kwa njia ya maofisa wetu wa habari, matangazo ya radio, kuwatembelea wakulima n.k. wakuu wa Mikoa ni wajibu wao kutusaidia katika jambo hili ili tupate mafanikio makubwa zaidi.

(f) **Magendo :**

Jambo hili hufanywa na wafanya biashara wa kati wa zamani ambao hutoa bei nzuri kwa wakulima na kuepukana na utaratibu wa kuuza mazao kwa njia ya mlango mmoja ulio wazi. Wanaweza kufanikiwa kutoa bei nzuri zaidi kuliko Halmashauri kwa vile hawana gharama zozote kama zile za Halmashauri za kuhifadhi mazao katika ghala, kufukizia mazao dawa ili kuzuia madhara ya wadudu n.k. Karibu mazao yote yanayonunuliwa kwa njia ya magendo husagwa hapa nchini au husafirishwa katika nchi za jirani kama vile Kenya ambako bei ni za juu kwa ajili ya upungufu wa muda wa mazao ya nafaka. Halmashauri ya mazao inajitahidi kwa kadri iwezavyo kulivunjilia mbali jambo hili la biashara ya

magendo. Tumemwajiri ofisa wa upelelezi kuwasaka wadhalimu wanaoendesha biashara ya magendo. Tukitumia njia za elimu, bidii inazidi kuongezwa kuwatangazia watu kwa kadri iwezekanavyo katika radio, masomo ya watu wazima, mikutano pamoja na wakulima n.k. Wakuu wa Mikoa na Wabunge kadhalika wanaweza kusaidia kuwaeleza wakulima faida ya kuuza mlango mmoja ulio wazi na hasa kwa faida ya upeo mrefu wa maendeleo; Wajumbe wa Halmashauri za maendeleo, V.D.C. wana nafasi nzuri zaidi ya kupeleleza na kuwatambua wadhalimu wavunja sheria na wasikose kutoa habari polisi n.k. ili hatua zichukuliwe. Halmashauri inajitahidi kutimiza kwa mafanikio kazi iliyo muhimu kwa taifa. Kazi hii si nyepesi lakini kwa msaada wa ushirikiano kutoka katika kila sehemu inayoweza kusaidia na hasa kutoka kwa wale watu wanaokutana na wakulima na walaji kila mara, tunatumaini tutafanikiwa kulitokomeza jambo hili la biashara ya magendo.

SWALI LA 12.

JE, WATU WOTE WANAEWEZA KUJSAIDIA HALMASHAURI ?

Jibu lililo wazi ni "NDIYO," kwa vile Halmashauri ni chombo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi ni wajibu wa kila raia mwema kushirikiana na Halmashauri ili kuhakikisha kuwa tunapata mafanikio.

Ingawa mtu wa kati mnyonyaji kadidimizwa chini na Halmashauri, bado hajatoweka kabisa. Yungali anaranda randa huku na huko akiipikia majungu Halmashauri. Tunachotaka watu wote wafanye ni kushirikiana na Halmashauri kwa kuwakanusha watu hao wapotevu. Ni sheria kwamba mazao yote ni lazima yauzwe kwa Halmashauri kupitia kwa maajenti wake ambao ni vyama vya Ushirika na shirika za vyama hivyo. Mtu ye yote asiyeruhusiwa anavunja sheria. Watu wote wanaweza kusaidia Halmashauri kwa kuhakikisha kwamba mazao hayauzwi kwa njia ya magendo. Washirikiane na Halmashauri kuwashitaki wanunuzi wa magendo. Wahudhuri katika mikutano ya hadhara inayoitishwa na Halmashauri, na kuwa waaminifu na wadilifu wakati wowote wanapohusika na mazao yanayonunuliwa na Halmashauri. Kila mmoja wetu lazima aangalie kwamba mazao tunayoiuzia Halmashauri ni safi na yenye sifa zinazotakiwa. Kadhalika watu wote wanaweza kuisaidia sana Halmashauri kwa kutoa makosa na maoni juu ya siasa yake na kazi zake.

SWALI LA 13.

KWA NINI HALMASHAURI YA TAIFA YA MAZAO HAITOI MIKOPO KWA VYAMA VYA USHIRIKA ?

Ingawa kutoa msaada wa fedha kwa jamii ya wakulima wasio na rasli mali ni jambo bora na ingawa Halmashauri yetu inayahurumia

matatizo ya vyama vya ushirika, kutolewa kwa misaada moja kwa moja ni lazima kuepukwe na badala yake misaada kama hiyo ingefaa zaidi itolewe kwa njia ya Benki ya Shirika au kwa njia nyingine za kiserikali (kwa mfano Halmashauri za mikopo) ambazo zinaongoza shughuli za maendeleo au kutoa misaada kwa watu binafsi kwa mujibu wa maendeleo ya nchi kijumla.

Kuna sababu kubwa nyingi zinazozuia Halmashauri yetu isipewe madaraka ya kutoa mikopo au kuweka mali katika mipango ya maendeleo moja kwa moja.

Kwanza, Halmashauri ya Taifa ya Mazao si chama (au Halmashauri) kilichoundwa ili kupata faida. Serikali imeshaanzisha vyama au Halmashauri mbali mbali maalum ambazo kazi yake ni kupata faida na ingekuwa kukariri mambo ingekuwa Halmashauri ya Taifa ya Mazao ingejaribu kushindana na vyama hivyo — jambo mojawapo ambalo Tanzania haiwezi kulimudu katika hatua tuliyofikia kwenye maendeleo. Wala haiwi sawa kwa Halmashauri kutoa mikopo moja kwa moja kwa vyama vya ushirika kwa sababu haina watumishi wa kushughulikia kazi za kutolea mikopo hiyo, na pia Benki ya Ushirika na Halmashauri ya Taifa ya Mikopo ndizo zinazohusika hasa na kazi hiyo.

Jambo la pili, Halmashauri ya Taifa ya Mazao inahitaji kukusanya rasli mali ya kutosha ili iweze kufanya shughuli zake vyema na kwa ujasiri, na ni sawa zaidi, kuziweka fedha hizo katika mkono wa serikali ili zitumike katika kazi za mpango wa maendeleo. Rasli mali inayowe kwa katika mali za serikali zinaweza kuchukuliwa, tena hazina hatari ya kupotea; jambo hilo haliwezi kuwa la kweli kwa kadri mikopo kwa Vyama vya Ushirika inavyohusika.

Mwisho Halmashauri ya Taifa ya Mazao kama Halmashauri ihusikanayo na masoko imeamriwa kukadiria kazi zake katika shughuli zile tu ilizowekewa kuzifanya, na kati ya shughuli hizo ilizopewa, ile ya kutoa misaada au mikopo kwa vyama vya ushirika haimo. Kwa hivyo basi haingekuwa sawa kwa Halmashauri ya Taifa ya Mazao kuchukuwa kazi hiyo mpya ya kutoa mikopo moja kwa moja kwa Vyama vya Ushirika.

SWALI LA 14.

**UUAZI WA MAZAO KWA KUFUATA SHERIA MAALUM,
UNA FAIDA AU HASARA GANI?**

Kuna sababu mbili kuu zinazosababisha uuzaji wa mazao kwa kufuata sheria maalumu. Sababu hizo ni za kisiasa na uchumi. Kwa

upande mmoja, kisiasa, mkulima wa kawaida ni muhimu sana hivi kwamba bidii ni lazima zifanywe ili kumfanya ajione kwamba kuwapo kwake kunatiliwa maanani na viongozi. Ingeleta hasara kwa siasa ya nchi angeachiliwa ajishughulikie yeye mwenyewe juu ya matatizo ya kuuza mazao na mahitaji badala ya kujibidisha katika kutoa mazao mengi zaidi kuliko anavyoweza kupata (uchumi) kwa jasho lake.

Pia kuna tatizo la uchumi ambalo ni lazima likabiliwe na ambalo linazidi kumpa mtu wazo la kujiuliza : “Je, ni kwa muda gani mpango huu wa kuhakikisha bei zilizolinganishwa na kurekebisha kwa misaada ya serikali utazidi kuendelea?” Kwa kadri uchumi unavyohusika, inaonekana kuwa kuna shauri la maana kupendelea uuzaji usio na vipingamizi mradi gharama ya shughuli zote haziwezi kupungua chini ya mpango wa kuweka bei maalum.

Kukadiria bei maalum katika hatua fulani fulani za uuzaji mara nyingi ni jambo linalofikiriwa sana katika uanzishaji wa Halmashauri za mazao. Halmashauri ya Taifa ya Mazao ilianzishwa hasa kwa kusudi la kurekebisha bei za mazao yaliyo chini ya uangalizi wake. Kwa hiyo, chini ya mpango wa kuuza mazao kwa kufuata sheria maalum, zinaweza kuanzishwa kwa urahisi njia njema na nyepesi zaidi za kuuza mazao; kwa kuondoa tofauti za bei anazopewa mkulima na kipato chake anahakikishiwa kwa kuwa uuzaji wa mazao yote ya kilimo unafuata mpango maalum na mwishowe faida kubwa inapatikana kwa kuweka nafasi moja kubwa ya kuuza vitu kwenye soko moja.

Sababu nyingine ya kuuza mazao kwa kanuni fulani chini ya Halmashauri za mazao — haihusu swali la uchumi bali linahusu jamaa au watu; siasa za utaiifa mahali au katika sehemu ambako biashara fulani mwanzoni zilikuwa mkononi mwa wafanya biashara waliokuwa wakipeleka faida (walizozipata) katika biashara walikuwa ni wa mataifa mengine tu, mahali hapo pamelazimu mabadiliko hayo ya uuzaji wa mazao ya mkulima yafanywe na Halmashauri za mazao. Ili kuondolea mbali makabila au watu wa kati (middlemen) na kuanzisha lengo maalum, kazi fulani fulani za biashara zimehamishwa na kuweka chini ya shughuli mojawapo ya serikali kuu, kwa mfano Halmashauri ya Taifa ya Mazao, Halmashauri ya Kahawa, Halmashauri ya Kuuza Pamba na Mbegu.

Mwishowe, hati ya kuziweka bei za vyakula vya lazima chini ya kima halisi imefanya serikali kuchukua madaraka ya kuongoza shughuli za uuzaji kwa mpango wa Halmashauri za mazao. Kati ya haja au mambo yanayosababisha kubadilika kwa bei pamoja na matokeo ya mabadiliko hayo kwa wakulima na walaji yanajulikana na wengi kati yenu mnaosoma karatasi hii. Ushahidi uliopo juu ya mawazo yaliyo-

potoka ambapo wanunuzi hufanya mambo bila kukadiria mipango ya bei za mazao, na pia bila kufikiria vile wanunuzi wengine wanaoshiriki wanavyoweza kufanya, jambo ambalo huzidisha mabadiliko ya bei. unaleta sababu nyingine ya kuingilia katika kurekebisha bei.

Hasara : (Juu ya kuweka kanuni maalum za uuzaji)

Kuna ubishi mwingi unaotolewa katika kupinga uwekaji wa kanuni maalumu za kufuatwa katika uuzaji.

Kwanza, inasemwa kwamba utumishi wa vifaa vya uchumi unaingiliwa. Inasemwa zaidi kuwa jambo hilo litazuia maendeleo ya uchumi kwa sababu nafasi za kutokutumia vyema mali au kugawanya ovyo uchumi zitaongezeka. Maelezo yanayoandamana na ubishi huu ni kwamba washindani nia yao claima ni kupata faida za namna mbali mbali. Kwa hivyo ni jambo lisiloepukika kwamba katika mpango wa biashara za masoko ni wale tu wanaojiweza kufanya kazi zao kwa gharama ndogo sana wanaoweza kuendelea. Hilo ni jambo lililo muhimu sana kwa mazao kama Mahindi ambayo hupatikana kwa wingi au uchache kwa kufuatana na hali ya hewa, jambo ambalo linahusu pia mazao mengine yanayopatikana kwa kilimo. Kwa jinsi uuzaji utakavyofanywa bila kuwekwa kanuni maalum, bei zitabadilika badilika kwa kufuatana na wingi wa mazao — zikiwa ndogo (au za chini) katika miaka ya neema, na zikipanda (kuwa juu) miaka mibaya.

Pili : Katika mpango wa kuweka kanuni maalumu za uuzaji, inazidi kusemwa kwamba hakuna kishawishi kwa kufanya kazi hora na kwa hiyo gharama za uuzaji zinabakia kuwa kubwa. Kwa hiyo katika miaka ya neema ambapo bei zingalikuwa ndogo kwa ajili ya mavuno makubwa, Halmashauri ya Taifa ya Mazao inapoteza fedha nyingi sana katika kutoa misaada kwa kuongeza fedha za malipo kwa mkulima, labda iwe kwamba bei za vitu kwa walaji ziwe zimewekwa juu makusudi kuliko zingelivyokuwa iwapo mazao na mahitaji yangukuwa ndiyo matatizo pekee yanayokabili kima cha bei.

Jambo la tatu : Bei aliyohakikishiwa mkulima pia inamfanya asishawishike kupunguza gharama za kazi ili kutoa mazao bora yatakayoleta faida kubwa, au kwenda kwenye shughuli zingine ambako angetoa mazao yatakayomletea faida.

Jambo la nne : Matokeo ya bei zilizokadiriwa kwa vyakula ni kuongeza gharama za watumishi. Mahindi na Mpunga ambavyo ni vyakula vya kila siku kwa wafanya kazi, ikiongezwa bei itaongeza pia mishahara na kwa jinsi hiyo itapunguza faida ya watumishi wa viwandani, au gharama ndogo ya utumishi ndicho kiini cha uendeshaji wa viwanda katika nchi zinazoendelea. Ni katika sababu hii pia ambamo mpango wa kuweka sheria au kanuni maalumu za uuzaji unasemwa kuwa unachelewesha maendeleo ya uchumi.

SWALI LA 15.**JE, NI SEHEMU GANI ITAKAYOCHUKULIWA NA HALMASHAURI
KATIKA MPANGO WA MIAKA MITANO ?**

Halmashauri ya Taifa ya Mazao kama vile Halmashauri nyingine za mauzo ni chombo cha kuondoa wasi wasi katika uchumi wa Taifa unaotokana na kuanguka anguka kwa bei. Kwa mpango wa kuwa na mfuko wa akiba wa kurekibisha bei Halmashauri inavunja hatari ya tofauti za bei zinazopatikana kwa kuuza mazao katika masoko ya nchi za nje na bei ya kununulia mazao. Pia inavunja hatari ya mabadiliko ya bei kati ya misimu. Zaidi ya hapo inalinda utaratibu wa mauzo wakati wa musimu. Kadhalika Halmashauri inafanya kazi za ustadi, biashara na mapesa.

Ustadi :

Kuyapanga mazao katika daraja ili kuhakikisha kuwa sifa za mazao zinazotakiwa zinapatikana. Haja yake ni kuinua sifa za mazao na kupata kwa jumla thamani kubwa ya mazao.

Biashara :

Inathibitisha kwamba wafanya biashara hawapati faida wasio-stabili kutokana na mazao hivyo huzuia ule unyonyaji wa watu wa kati.

Mapesa :

Inatunza schemu fulani ya fedha zinazotokana na mauzo ya mazao kwa nchi za nje ambazo angelilipwa mkulima na huzitumia fedha hizo kwa matumizi mengine kama vile matumizi ya Halmashauri kuhusu mambo mbali mbali ya mipango ya maendeleo (kwa mfano, kuhifadhi mazao katika ghala) au kuzihamisha pesa toka kwenye Halmashauri kwenda serikalini kwa matumizi ya kuendeshea mipango ya jumla ya maendeleo.

Uthabiti wa bei unawatia moyo watu waongeze mazao yao na kufanya maamuzi bora juu ya fedha. Baadhi ya mazao yanauzwa kwa kufuata utaratibu wa sheria za serikali yanachukua sehemu kubwa sana ya mazao yauzwayo nchi za nje na kuingiza fedha nchini, hivyo kazi za Halmashauri ya Taifa ya Mazao ni za maana sana katika uchumi wetu wa Taifa. Kwa hiyo Halmashauri ya Taifa ya Mazao ikiwa ni chombo cha kuendeshea uchumi inarekibisha bei za mazao, huwaondosha wafanya biashara wa kati, huwalinda wakulima katika dhoruba ya mashindano na nchi za kigeni na walaji wasidhulumawe na wanyonyaji.

Zaidi ya hapo, Halmashauri ya Taifa ya Mazao — kama vyombo vingine vya uchumi husaidia katika kujenga uchumi kwa njia nyingine nyingi. Huhifadhi baadhi ya fedha zake kwa matumizi ya kukuza na kuendeleza kazi zake k.m. kutumia fedha katika kuongeza nafasi za ghala, majengo na vifaa. Pia huwarudishia wakulima faida au sehemu ya faida (kwa njia ya malipo ya pili). Tatu, kwa vile Halmashauri inachukua fedha zinazohitajika kwa matumizi yake ambayo ni madogo sana inafanya walaji wapate bei nafuu na utumishi bora — kawaida yetu ni kumwuzia mlaji bei ya chini na kuwalipa wakulima bei ya juu.

Halmashauri ya Taifa ya Mazao inachukua sehemu ya maana sana katika kujenga msingi wa uchumi katika Jamhuri yetu kwa kurekibisha bei za mazao ya kilimo yanayouzwa kwa kufuata taratibu za sheria za serikali; na mumo kwa mumo husaidia kurekibisha mapato ya wakulima, serikali na biashara na nchi za nje.

SWALI LA 15.**JE, NI SEHEMU GANI ITAKAYOCHUKULIWA NA HALMASHAURI
KATIKA MPANGO WA MIAKA MITANO ?**

Halmashauri ya Taifa ya Mazao kama vile Halmashauri nyingine za mauzo ni chombo cha kuondoa wasi wasi katika uchumi wa Taifa unaotokana na kuanguka anguka kwa bei. Kwa mpango wa kuwa na mfuko wa akiba wa kurekibisha bei Halmashauri inavunja hatari ya tofauti za bei zinazopatikana kwa kuuza mazao katika masoko ya nchi za nje na bei ya kununulia mazao. Pia inavunja hatari ya mabadiliko ya bei kati ya misimu. Zaidi ya hapo inalinda utaratibu wa mauzo wakati wa musimu. Kadhalika Halmashauri inafanya kazi za ustadi, biashara na mapesa.

Ustadi :

Kuyapanga mazao katika daraja ili kuhakikisha kuwa sifa za mazao zinazotakiwa zinapatikana. Haja yake ni kuinua sifa za mazao na kupata kwa jumla thamani kubwa ya mazao.

Biashara :

Inathibitisha kwamba wafanya biashara hawapati faida wasio-stahili kutokana na mazao hivyo huzuia ule unyonyaji wa watu wa kati.

Mapesa :

Inatunza sehemu fulani ya fedha zinazotokana na mauzo ya mazao kwa nchi za nje ambazo angelilipwa mkulima na huzitumia fedha hizo kwa matumizi mengine kama vile matumizi ya Halmashauri kuhusu mambo mbali mbali ya mipango ya maendeleo (kwa mfano, kuhifadhi mazao katika ghala) au kuzihamisha pesa toka kwenye Halmashauri kwenda serikalini kwa matumizi ya kuendeshea mipango ya jumla ya maendeleo.

Uthabiti wa bei unawatia moyo watu waongeze mazao yao na kufanya maamuzi bora juu ya fedha. Baadhi ya mazao yanauzwa kwa kufuata utaratibu wa sheria za serikali yanachukua sehemu kubwa sana ya mazao yauzwayo nchi za nje na kuingiza fedha nchini, hivyo kazi za Halmashauri ya Taifa ya Mazao ni za maana sana katika uchumi wetu wa Taifa. Kwa hiyo Halmashauri ya Taifa ya Mazao ikiwa ni chombo cha kuendeshea uchumi inarekibisha bei za mazao, huwaondosha wafanya biashara wa kati, huwalinda wakulima katika dhoruba ya mashindano na nchi za kigeni na walaji wasidhulumliwe na wanyonyaji.

Zaidi ya hapo, Halmashauri ya Taifa ya Mazao — kama vyombo vingine vya uchumi husaidia katika kujenga uchumi kwa njia nyingine nyingi. Huhifadhi baadhi ya fedha zake kwa matumizi ya kukuza na kuendeleza kazi zake k.m. kutumia fedha katika kuongeza nafasi za ghala, majengo na vifaa. Pia huwarudishia wakulima faida au sehemu ya faida (kwa njia ya malipo ya pili). Tatu, kwa vile Halmashauri inachukua fedha zinazohitajika kwa matumizi yake ambayo ni madogo sana inafanya walaji wapate bei nafuu na utumishi bora — kawaida yetu ni kumwuzia mlaji bei ya chini na kuwalipa wakulima bei ya juu.

Halmashauri ya Taifa ya Mazao inachukua sehemu ya maana sana katika kujenga msingi wa uchumi katika Jamhuri yetu kwa kurekibisha bei za mazao ya kilimo yanayouzwa kwa kufuata taratibu za sheria za serikali; na mumo kwa mumo husaidia kurekibisha mapato ya wakulima, serikali na biashara na nchi za nje.